**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Zanzibar*
*18 Januari, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI
## SALAMU ZA RAMBIRAMBI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametuma salamu za rambirambi kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mussa Azzan Zungu, kufuatia kifo cha Mhe. Halima Idd Nassor, Mbunge wa Viti Maalum wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupitia kundi la Wafanyakazi, kilichotokea leo tarehe 18 Januari, 2026.

Mhe. Halima Idd Nassor amefariki dunia akiwa anapatiwa matibabu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili – Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI). Mazishi yanatarajiwa kufanyika leo tarehe 18 Januari, 2026, Kigamboni, Jijini Dar es Salaam.

Rais Dkt. Samia ameeleza Marehemu alikuwa kiongozi mwenye mchango mkubwa kwa Chama na Taifa, hususan katika kutetea maslahi ya kundi la wafanyakazi na kuchangia maendeleo ya jamii kupitia majukumu yake ya kibunge na ndani ya Chama Cha Mapinduzi.

Rais Dkt. Samia anatoa pole kwa familia ya Marehemu, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) pamoja na wanachama wote wa Chama Cha Mapinduzi (CCM); Waheshimiwa Wabunge, na ndugu, jamaa na marafiki kwa msiba huu mzito.

Halikadhalika, Rais Dkt. Samia anawaombea subira, faraja na nguvu wafiwa wote, na kumuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu